Maswali

1. Nani alikuwa mfalme muovu? Alifanya nini iliyokuwa ovu?
2. Nani alikuwa nabii wa Mungu?
3. Mungu alifanya nini kama adhabu kwa sababu Ahabu na watu wa Israeli walifanya maovu?
4. Mungu alilinda Eliya. Mungu aliambia Eliya kwenda wapi mara ya kwanza?
5. Kule Eliya alipata chakula namna gani?
6. Mungu aliambia Eliya afanye nini Kijito kilipo kauka?
7. Eliya aliuliza huyo mwanamke mjane afanye nini?
8. Mjane alimjibu nini?
9. Mungu alilinda Eliya, mjane na mwanawe namna gani?
10. Eliya alifanya nini mwana wa yule mjane alipokufa?

Majibu

1. Ahabu alikuwa mfalme muovu. Aliabudu Baali tena alifundisha watu wa Israeli waabudu Baali.
2. Eliya alikuwa nabii wa Mungu.
3. Mungu alisema hakutakuwa na mvua. Kulikuwa na njaa kubwa.
4. Mungu aliambia Eliya aende kwa Kijito cha Kerithi.
5. Kunguru walileta mkate na nyama kila asubuhi na jioni.
6. Mungu aliambia Eliya aende kwa mji wa Sarepta.
7. Eliya aliuliza maji ya kunywa na mkate.
8. Alikuwa na unga kidogo na mafuta ya chakula kimoja wale halafu yeye na mwanawe wafe.
9. Mungu hakuacha unga na mafuta zikwishe. Kulikuwa na cha kutosha kwa kila siku.
10. Eliya aliomba Mungu na kujinyorosha kwa kijana. Alimrudishia uhai tena.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2

69 Mungu analisha Eliya

Kwa Biblia

1 Wafalme mlango wa 17

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu analinda wale wanaompenda na kumwamini

Somo

Ahabu alikuwa mfalme wa Israeli. Alikuwa muovu sana. Ahabu aliabudu mungu wa uongo, Baali. Aliwafundisha watu wa Israeli kuabudu Baali. Eliya alikuwa nabii wa Mungu. Eliya aliabudu Mungu. Mungu alikasirika kwa sababu Ahabu na watu wa Isaeli waliabudu Baali. Mungu alituma Eliya aambie Ahabu, “Wewe na Waisraeli mnaabudu Baali. Mnafanya mambo mengi maovu. Kwa hivyo hakutakuwa na mvua mpaka nimwambie.”

Mungu hakuleta mvua yoyote kwa hiyo nchi. Mimea ilikauka. Hakukuwa na chakula. Kulikuwa na njaa kuu. Mfalme Ahabu aliudhika sana.

Mungu analinda wote wanaompenda na kumwamini. Mungu alificha Eliya kutoka kwa Ahabu. Mungu alimwambia aende ajifiche karibu na kijito (mto) kinachoitwa Kerithi. Mungu aliahidi kwamba atatumia Eliya chakula.

Eliya alikaa karibu na kijito cha Kerithi. Alikunywa maji kutoka kwa hicho kijito. Kila asubuhi na jioni, Mungu alituma kunguru (ndege weusi wakubwa) waletee Eliya mkate na nyama. Hakukuwa na chakula kilichokua kwa nchi iliyokauka. Lakini Eliya alikuwa na chakula kila siku. Mungu alituma kunguru waletee Eliya mkate na nyama.

Hakukuwa na mvua kwa muda mrefu. Kijito cha Kerithi kilianza kukauka. Bunde tu, Eliya atakosa maji ya kunywa. Eliya alijua kwamba Mungu atamlinda. Aliongoja kwenye kijito mpaka Mungu alipomwambia cha kufanya.

Mungu alimwambia Eliya, “Enda kwa mji wa Sarepta na uishi kule. Nimemwaagiza mwanamke mjane akulishe.” Ilikuwa safari ndefu kwenda Sarepta. Eliya alisafiri kupitia katikati ya nchi ya Israeli. Sarepta ilikuwa kwa nchi moja ya Israeli. Ilikuwa safari ya hatari. Wapelelezi wa Ahabu walikuwa wakimtafuta. Lakini Eliya aliamini kwa Mungu. Alifika Sarepta salama.

Eliya alipitia kwa lango la mji. Aliona yule mwanamke mjane akiokota kuni. Akaita yule mjane. Alimuuliza ampe maji ya kunywa na mkate. Lakini njaa ilikuwa kwa hiyo nchi pia. Yule mwanamke akaambia Eliya, “Sina mkate wowote. Nina tu unga kidogo kwa pipa na mafuta kidogo kwa chupa. Niko naokota kuni kidogo niende nikapike chakula nikule na mwanangu. Baadaye hatutakuwa na kingine. Tutakufa.”

Eliya aliambia yule mjane, “Usiogope. Enda nyumbani unipikie mimi mkate kwanza. Uniletee huo mkate. Baadaye ujipikie wewe na mwanao. Kwa maana hii ndiyo Bwana, Mungu wa Israeli anasema, Unga ulio kwa pipa hautaisha. Chupa ya mafuta haitakauka mpaka Mungu alete mvua kwa nchi.’”

Yule mjane aliamini Eliya. Aliamini kwamba Mungu atawalinda na kuwalisha. Yule mjane alitumia unga wote na mafuta kutengenezea Eliya mkate.

Alipelekea Eliya mkate. Yule mjane alipoenda kutengeneza mkate ale na mwanawe – kulikuwa na unga kidogo tena kwa pipa. Hata kwa chupa kulikuwa na mafuta kidogo!

Mungu alilinda Eliya, yule mjane na mwanawe. Kila asubuhi yule mjane alitengenezea Eliya mkate. Tena alitengeneza yake na mwanawe. Kila siku Mungu aliwalinda. Wakati wote kulikuwa na unga kidogo kwa pipa na mafuta kidogo kwa chupa. Eliya aliishi kwa muda mrefu na mwanamke mjane pamoja na mwanawe.

Siku moja mwana wa yule mjane alikuwa mgojwa sana. Aliendelea kudhoofika. Baadaye akafa. Yule mjane alihuzunika sana. Akakasirika. Alikuwa amesaidia Eliya na sasa mwanawe amekufa. Eliya aliambia yule mjane, “Nipe huyo mtoto wako.” Eliya alibeba mtoto aliyekufa hadi kwa chumba chake. Alimlaza kwa kitanda. Eliya aliomba Mungu. Eliya alijinyorosha mara tatu kwa mwili wa maiti. Aliomba Mungu, “Ee Bwana Mungu wangu, rudishia huyu kijana uhai wake.”

Mungu alisikia maombi ya Eliya. Mungu alirudishia huyo kijana uhai tena. Eliya alimrudisha kwa mamake. Alisema, “Angalia, mwanao yu hai tena!”

Yule mwanamke mjane alifurahi sana. Alisema, “Sasa najua wewe ni mtu wa Mungu. Neno la Mungu lolote usemalo ni la kweli.”